# Wizara ya Mifugo na Uvuvi, ilivyojidhatiti kuboresha afya ya jamii

NA. OMARY MTAMIKE, UVUVI

KATIKA jamii zetu tumezoea kutumia nyama kama kitoweo aidha kwa mtu mmoja mmoja, familia au kunapokuwa na mkusanyiko wa watu wakati wa tukio la furaha au majonzi na mara nyingine wanyama hawa hutumika kama ishara ya ukarimu pindi familia inapotembelewa na wageni.

Upeo wa usalama wa kitoweo hicho kwa mnunuzi huishia buchani au sokoni na wasichokijua wengi ni kuwa hiyo huwa ni hatua ya mwisho kwani tayari anakuwa ameshapitia hatua zote za uhakiki wa usalama wake kwa mlaji mpaka anaingia sokoni.

Zipo sheria na taratibu kadhaa zinazoziongoza mamlaka za Serikali katika kuhakikisha nyama inayomfikia mlaji inakuwa ni salama na kwa upande wa vyakula vya Mifugo ambavyo ndio msingi wa ubora wa mnyama anayepelekwa sokoni ipo sheria ya Nyanda za malisho na chakula cha mifugo ya mwaka 2010 pamoja na kanuni zake zilizoandaliwa mwaka 2013.

Sheria hizo zinawapa mamlaka wakaguzi wa vyakula hivyo kwenda kuhakiki ubora wa mazingira ya uandaaji wa vyakula hivyo, uwiano stahili wa viinilishe vilivyopo katika vyakula hivyo na uwepo wa ithibati ya ubora wa kila kundi la vyakula vinavyoandaliwa.

[illegible] la msingi [illegible] ya wataalam wa ukaguzi wa vyakula vya Mifugo huungana na wataalam wenzao kutoka Wakala ya

> Upeo wa usalama wa kitoweo hicho kwa mnunuzi huishia buchani au sokoni na wasichokijua wengi ni kuwa hiyo huwa ni hatua ya mwisho kwani tayari anakuwa ameshapitia hatua zote za uhakiki wa usalama wake kwa mlaji mpaka anaingia

Shot on AWESOME A70




*MTENDAJI Mkuu wa Wakala wa Maabara ya Veterinari nchini (TVLA) Dk. Stella Bitanyi akitoa taarifa fupi ya operesheni ya siku 2 ya ukaguzi wa viwanda na maduka yanayouza vyakula vya Mifugo ofisini kwake jijini Dar-es-Salaam*

kwenye operesheni hiyo waliwapa ushauri wa kitaalam juu ya mambo ya kufanya katika

Mkuu wa Wakala ya Maabara ya Veterinari nchini (TVLA) wenye ithibati ya kitaifa ya kuchambua

wizaramifugouvuvi.go.tz ambako watapata maelekezo yote ya namna ya kuisajili au kuhuisha

CamScanner

# Wanawake wawezeshwa kushiriki ufugaji kisasa

**NA MWANDISHI WEU**

OFISA Kilimo, Mifugo na Uvuvi Manispaa ya Kahama, Richard Hegera, amewataka wanakikundi cha Wanawake cha Busabi, kuitumia vizuri elimu ya ufugaji kuku waliyopewa kubadili maisha yao.

Hegera alisema hayo jana, katika Kata ya Mondo, wilayani Kahama, alipokabidhi mradi wa kisasa wa ufugaji kuku wa mayai baada ya kupewa mafunzo na mitaji kutoka mgodi wa Barrick Buzwagi.

Alisema hatua zilizochukuliwa na mgodi huo kuwasaidia wajasiriamali kwamba mradi huo utawasaidia kubadilisha maisha ya familia za wanakikundi hicho na taifa.

"Naishukuru kampuni ya Barrick kwa kuchukua hatua hiyo na kwamba mradi huo utasaidia kubadilisha maisha ya familia za wanakikundi hawa na taifa kwa ujumla," alisema.

Kwa upande wake Meneja wa Mgodi wa Buzwagi, Rebecca Stephen, alisema utekelezaji wa mradi huo ni sehemu ya miradi iliyopo katika mpango wa kufunga mgodi wenye lengo la kuwawezesha wanawake na vijana kuwa na maisha endelevu, kwa sababu wengi wao walitegemea kuendesha maisha kutokana na mgodi huo.

Alisema pamoja na kuwapa mtaji wanachama wa kikundi hicho, Barrick iliwawezesha kwa mafunzo ya vitendo na nadharia ya [illegible]ku kwa njia za kisasa na kuunganishwa na soko la pamoja ndani ya mgodi huo.

UCHUMI

# Mradi Uvuvi ulivyoleta maisha mapya kwa wavuvi Victoria

**Na Neema Emmanuel, MWANZA**

NI zaidi ya nuru jua la siku nzima kugeuka historia, kazi kufanyika kwa saa 12 bila ya kutetereka. Sasa ni zamu ya wavuvi kutoka mwalo wa Igombe Kayenze ndogo wilayani Ilemela, vilio vyao vya kupoteza maisha kwa mlipuko wakiwa ziwani, dagaa kusombwa na maji ,kukosa ubora ,kushinda juani sasa basi.

Frank Faustine, mvuvi wa dagaa kwa zaidi ya miaka 15 akieleza Nipashe adha walizokuwa wakikumbana nazo wakati wakitekeleza majukumu yao ya uvuvi wa dagaa Ziwa Victoria.

Anasema, kupoteza maisha wakiwa katika majukumu yao ni jambo la kawaida, akifafanua wanavyopoteza Maisha, taa za kuvua aina ya koroboi zinazotumia mafuta ya taa ndio chanzo kikuu, kwani kuna wakati zinalipuka na kusababisha ajali.

Ni mlipuko unaochangiwa kwa kiasi kikubwa na mafuta ya petroli yanayoyatumika kuendesha mitumbwi yao.

Pia, anaeleza kuwa koroboi hizo ni chanzo kikubwa cha madhara kwa viumbe majini, kwa sababu mwanga wake ulikwenda chini, hivyo ujio wa taa za nishati ya jua za kuvulia samaki na dagaa, sam-



Wavuvi wakiweka taa zinazotumia nishati ya jua kwenye mitumbwi yao kwa ajili ya kwenda kuvua dagaa. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

saa 12 jioni hadi 12 asubuhi, mwanga ukiwa ni uleule tofauti na awali taa ziliwaka kwa saa sita, baada ya hapo mwanga unapungua na kuwa hafifu, hata wanashindwa kufanya ni mwendo wa kazi tu," anaeleza Faustine.

**MKAUSHA SAMAKI**

Anna Said, mkaushaji dagaa ka-

mradi mpya ni ukombozi katika biashara zao.

Anasema mvua ni hatari kwa dagaa wanaponyeshewa, wanaoza ikizingatiwa maeneo yao walikuwa

limradi huu uwe endelevu na usije ukaishia njiani ili uweze kutuokoa na kuinua kiuchumi kwa sababu hapa dagaa zinakaushwa kwa muda mfupi, tena sio kwa uwazi.

"Hata kama mvua ikinyesha zipo salama, zinaoshwa vizuri na wanaweka chumvi na kuzifanya zikae kwa muda mrefu tofauti na zile zetu za awali," anaeleza said.

Aidha, Johness Mashange ni Mwenyekiti wa Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi ndani ya mita 60 kutoka mwambao mwa ziwa (BMU) na mwenyekiti wa wavuvi Kanda ya Ziwa, anaeleza kuwa teknolojia hiyo inaleta mabadiliko na tija kiuvuvi kwa sababu mwanga wake umefanyiwa utafiti mavuno uzalishaji unaongezeka kwa wingi hivyo wanaendelea kuwahamasisha wavuvi watumie njia hiyo bora kwa manufaa yao na kukuza uchumi wa nchi.

**BOSI KIWANDANI**

Diana Mbogo ni Mkurugenzi Mkuu wa kiwanda cha ukaushaji na uchakataji dagaa, Millennium Engineers anaeleza kuwa mradi wa kukausha dagaa kwa kutumia mtambo wa umeme jua

...za kuwa kamp... ufadhili wa seri... akala wa Nishati ...EA ), wamewale... na mitambo ...ambayo ni ya kwa... ashariki inayosa... dagaa tani 1.2 ... fupi na kuzifa... ubora unaokidh... a kimataifa.

...analitaja ni ku... na matumizi ... ambayo inata... adhara mbalim... mlipuko na k... maisha wavuv...

Shot on AWESOME A70

CamScanner

# Govt empowers artisanal fishermen

THE government is implementing a Blue Economy Intervention Plan that aims at empowering artisanal fishermen in the country, the House of Representatives was told here yesterday.

Blue Economy and Fisheries Minister, Suleiman Masoud Makame told the house that in the plan execution, the ministry has started providing fishermen with seven and eight-metre fishing boats.

During the second phase, fishermen will be given the fishing vessels as per their demand and capacity, said the minister.

He further added that the government under the International Fund for Agricultural Development (IFAD) project plans to procure four fishing ships, starting with one vessel, which will be used for training of wananchi on deep sea fishing.

Minister Makame was answering a question by Mwanakwerekwe Representative Ameir Abdalla Ameir who sought to know the government strategies to enable artisanal fishermen grow from their small scale into deep sea fishing.

CamScanner

# Mwakilishi ashtukia kasi uvuvi haramu

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wameitaka Wizara ya Uvuvi na Uchumi wa Buluu kudhibiti matukio ya uvuvi haramu yanayotishia uhai wa viumbe vya baharini na maliasili za matumbawe.

Akichangia Muswada wa kuanzishwa kwa Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za baharini, Mwakilishi wa Jimbo la Kojani, Hassan Omar Hamad (ACT-Wazalendo) alisema kumejitokeza kasi ya matukio ya uvuvi haramu unaotishia maisha ya viumbe vya baharini ambapo mitego inayotishia maisha ya samaki ndiyo inayotumika kwa sasa.


Alitaka wizara hiyo kupiga marufuku nyavu zenye macho madogo ambazo ni tishio huku zikinasa samaki wa aina mbalimbali ikiwamo wadogo ambao hawafai kwa matumizi ya kula.

Alizitaja nyavu za kukokota baharini ambazo huharibu matumbawe ambayo ni mazalia ya samaki pamoja na aina mbalimbali za majani ambayo ni chakula cha samaki.

"Wizara ya Uvuvi na Uchumi wa Buluu tunaomba waje na orodha ya aina zote za uvuvi ikiwamo ambazo hazifai kwa matumizi ya shughuli za baharini kwa sababu hivi sasa kumejitokeza uvuvi haramu unaotishia uhai wa viumbe vya baharini," alisema.

Aidha, Mwakilishi wa Jimbo la Ziwani, Suleiman Makame Haji (CCM) alisema kuwepo kwa Sheria ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za bahari ni muhimu ambao itawezesha kujua kiwango cha samaki kilichopo kwa ajili ya matumizi.

Alisema utafiti wa aina hiyo unahitajika ambazo zitakuja na jawabu sahihi kujua utajiri wa samaki



waliopo pamoja na aina nyingine za samaki zilizo katika tishio la kutoweka.

"Baadhi ya aina ya samaki ambao ni maarufu wameanza kupungua hatua kwa hatua ambapo huu ni wakati mwafaka tuje na jawabu sahihi kujua sababu zake baada ya kufanya utafiti," alisema.

Alitaja baadhi ya samaki ambao utafiti unahitajika kubaini sababu za kupungua kwake ikiwamo pweza, ngisi pamoja na kamba ambao ni maarufu kwa soko la watalii ikiwa pia ni samaki wenye kuingiza lishe mwilini.

Mwakilishi wa Jimbo la Bumbwini, Mtumwa Peya Yussuf (CCM) aliitaka Taasisi za Uvuvi wa Bahari kuja na utafiti utakaoonesha mahitaji ya kilimo cha mwani na mazao mengine ya baharini.

Alisema mwani unakabiliwa na mabadiliko ya tabia ya nchi ambapo uzalishaji wake umepungua, hivyo utafiti zaidi unahitajika kukabiliana na changamoto hizo.

"Tunahitaji kufanya utafiti ambao utatuwezesha kujua changamoto zinazokabili kilimo cha mwani, kupungua uzalishaji wake kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi," alisema.

Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kauli moja walipitisha muswada huo ambao pamoja na mambo mengine utaweka masharti yanayohusiana na kuendesha shughuli za uvuvi baharini katika maeneo ya hifadhi.

# Kilio soko la samaki kisikike sasa

Kanda ya ziwa hakupo shwari. Mwenendo wa soko la samaki unazidi kuleta hofu kwa wadau mbalimbali wa sekta hiyo katika ukanda huo.

Kuna kilio cha upungufu wa samaki katika Ziwa Victoria, hali inayoelezwa kusababishwa na uvuvi haramu, mrundikano wa tozo na matumizi ya taa za betri.

Sababu hizi ni kwa mujibu wa wavuvi na ndizo zinazochangia soko la bidhaa hiyo kuporomoka.

Kwa mujibu wa ripoti ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kuhusu ufanisi wa uchumi wa kanda iliyotolewa Oktoba 5 mwaka huu, licha ya uuzaji wa samaki Kanda ya Ziwa kuongoza nchini, uuzaji huo umepungua ikilinganishwa na miaka minne iliyopita.

Ripoti hiyo ilionyesha mauzo ya samaki kwa ujumla nchini yameongezeka kufikia tani 94,544.8 mwaka 2022/2023, ikichangiwa na ongezeko la kanda ya Kusini Mashariki, lakini Kanda ya Ziwa yamepungua kutoka tani 34,863.9 mwaka 2019/20 kufikia tani 27,548.6 mwaka 2022/23.

Ni kwa sababu hiyo, hata mapato yatokanayo na samaki yaliathirika, kwani takwimu zinaonyesha mauzo yake mwaka 2022/2023 yalikuwa Sh506.8 bilioni, yakipungua kutoka Sh526.5 bilioni mwaka 2021/202.

Ukiondoa sababu hizo za kushuka kwa uzalishaji wa samaki, jambo lingine linalotajwa kama sababu ya kuonekana kuwa uzalishaji umeshuka, ni kitendo cha wavuvi kuamua kuuza mazao yao ya samaki kwenye masoko ya ndani, wakidaiwa kukwepa kuuza viwandani kulingana na malipo kuwa chini, hivyo kusababisha Serikali isipate takwimu sahihi za mauzo ya kitoweo hicho.

Kimsingi, bei halisi ya viwandani haiendani na uendeshaji kazi wa wavuvi, kwa hiyo wavuvi wanaona kuliko kuuza kwa kilo moja hadi nne kuanzia Sh11,000, ni bora wapasue samaki zao watoe mabondo, wauze mabondo halafu wauze minofu ambapo wanapata faida zaidi na hivyo kuwa na moyo wa kuendelea na shughuli yao ya uvuvi.

Tunatambua kuwapo mipango na mikakati mbalimbali ya Serikali kupitia wizara husika ya uvuvi na mifugo katika kudhibiti uvuvi haramu na hata kuweka mazingira bora ya kuhakikisha kuna uzalishaji wa samaki ziwani.

Hata hivyo, kwa kelele zinazopigwa na wavuvi muhimu, ni dhahiri kuna mambo hayako sawa. Hayo ndiyo yanayotusukuma kupaza sauti kwa niaba ya wavuvi kuwa Serikali inapaswa kuamka sasa na kusikiliza kero na vilio vya wavuvi.

Kwa mfano, wavuvi wanawezaje kufanya shughuli zao kwa ufanisi na tija ikiwa wanalia na uwepo wa tozo zaidi ya 10? Ikiwa tozo ni kikwazo katika uzalishaji wa samaki na hivyo kushusha soko lake na mapato kwa nchi, ni wakati mwafaka wa Serikali kuona haja ya kupunguza tozo hizo ili kuweka mazingira rafiki zaidi kwa wavuvi kuendelea na shughuli zao.

Tusikubali kuiacha sekta hii ikapwaya hasa kwa kuzingatia kuwa ni miongoni mwa sekta muhimu zinazoiletea nchi yetu mapato makubwa kila mwaka.

Hatuwezi kukuza mapato hayo ilhali wadau muhimu katika uzalishaji wa samaki, wana lundo la vikwazo wanavyodai kuwarudisha nyuma katika shughuli zao.





# Uvuvi haramu tishio uhai viumbe bahari, maliasili

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi, wameitaka Wizara ya Uvuvi na Uchumi wa Buluu, kudhibiti matukio ya uvuvi haramu ambayo yanatishia uhai wa viumbe vya baharini na maliasili za matumbawe.

Akichangia muswada wa kuanzishwa kwa taasisi ya utafiti wa uvuvi wa maliasili za baharini katika kikao cha baraza la wawakilishi jana, mwakilishi wa jimbo la Kojani, Hassan Omar Hamad, alisema kumejitokeza kasi ya matukio ya uvuvi haramu unaotishia maisha ya viumbe vya baharini na mitego tishio kwa maisha ya samaki inatumika kwa sasa.

Aliitaka Wizara ya Uvuvi kupiga marufuku nyavu zenye macho madogo ambazo zinanasa samaki wadogo ambao hawafai kwa matumizi ya kula.

Aidha, alizitaja nyavu za kukokota baharini kuwa huharibu matumbawe ambayo ni mazalia ya samaki pamoja na aina mbalimbali za majani ambayo ndiyo chakula cha samaki.

"Wizara ya uvuvi na uchumi wa buluu tunawaomba waje na orodha ya aina zote za uvuvi ikiwamo zile ambazo hazifai kwa matumizi ya shughuli za baharini kwa sababu hivi sasa kumejitokeza uvuvi haramu unaotishia uhai wa viumbe vya baharini," alisema. Mwakilishi wa Jimbo la Ziwani, Suleiman Makame Haji, alisema kuwapo kwa sheria ya utafiti wa uvuvi na maliasili za bahari ni muhimu ambao utawezesha kujua kiwango cha samaki kilichopo kwa ajili ya matumizi.

Alisema utafiti wa aina hiyo unahitajika na unakuja na jawabu sahihi kujua utajiri wa samaki waliopo pamoja na aina nyingine za samaki ambazo zipo katika tishio la kutoweka.

"Baadhi ya aina ya samaki ambao ni maarufu wameanza kupungua hatua kwa hatua na huu ni wakati mwafaka tuje na jawabu sahihi kujua sababu zake baada ya kufanya utafiti," alisema.

Aliwataja baadhi ya samaki ambao utafiti unahitajika ili kukabiliana na sababu za kupungua kwake ikiwamo pweza, ngisi na kamba ambao ni maarufu kwa soko la watalii ikiwa pia ni samaki wenye kuongiza lishe mwilini.

Mwakilishi wa Jimbo la Bumbwini, Mtumwa Peya Yussuf, aliitaka taasisi za uvuvi wa bahari kuja na utafiti utakao onesha mahitaji ya kilimo cha mwani na mazao mengine ya baharini.

Alisema mwani unakabiliwa na mabadiliko ya tabianchi kutokana na kupungua kwa uzalishaji na kwamba utafiti zaidi unahitajika kukabiliana na changamoto hizo.

"Tunahitaji kufanya utafiti ambao utatuwezesha kujua changamoto zinazokikabili kilimo cha mwani kupungua uzalishaji wake kutokana na mabadiliko ya tabianchi," alisema.

Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, walipitisha mswada huo ambao pamoja na mambo mengine utaweka masharti yanayohusu na kuendesha shughuli za uvuvi baharini katika maeneo ya hifadhi.